

## **Kanuni kuhusu mienendo na tabia ya ngono kwa wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu.**

Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **wanaweza kuadhibiwa - hata kufutwa kazi – kwa sababu ya tabia isiyokubalika inayohusiana na ngono**. Hizi ndizoambazo lazima wazingatia:

- Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **hawaruhusiwi kuwa na mahusiano ya kingono na mtu yeote mwenye umri chini ya miaka 18, hata kama sheria inaruhusu katika nchi yao**. Kusema haukujuwa umri halisi wa muhusika sio sababu ya kutosha.
- Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **hawaruhusiwi kulipia ngono kwa pesa, kazi, bidhaa au huduma** - ikiwa ni pamoja na kulipa kwa kutumia bidhaa na huduma zilizonuiwa kama msaada kwa watu wanaouhitaji. Hawapaswi kutoa ahadi za mambo haya ili kuwalazimisha watu wengine kukubali aina yoyote ya vitendo vitakavyowadhalilisha au kuwanyanya. Hii ni pamoja na kulipa au kutoa fedha kwa ajili ya kuwa na uhusiano wa kingono na kahaba.
- Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu wana ushawishi kuhusu nani atakayepokea bidhaa na huduma. Hii inawapa mamlaka katika masuala ya watu wanaohitaji misaada. Kwa sababu hiyo, mashirika ya kibinadamu **yanawahimiza vikali wafanyakazi wasiwe na mahusiano ya kingono na mtu yeote aliyeathirika** na majanga ya dharura. Mahusiano kama hayo yanafanya shughuli za mashirika ya kibinadamu kuonekana kuwa yasiyo aminifu na sio ya kuaminika.
- Kama mfanyakazi wa shirika la kibinadamu ana **wasiwasi au anashuku** kwamba kuna mfanyakazi katika shirika lake au shirika lingine la msaada ambaye inawezekana anavunja sheria za mashirika ya kibinadamu kuhusu maadili za kingono, **ni lazima** atoe taarifa, kuambatana na **taratibu** zilizowekwa na mashirika yao.
- Wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu **wanapaswa kujenga na kuendeleza mazingira ya kazi** ambayo yanazuia tabia za kingono zisizokubalika na kuwashimiza wafanyakazi kuwa na maadili nzuri inayoambatana na **kanuni za utendaji kazi . Wakurugenzi wote** wana wajibu wa kusaidia na kuendeleza mifumo inayohifadhi mazingira haya.

Kanuni za IASC kuhusu unyanyasaji na dhulma katika uhusiano wa kingono zinapatikana hapa:

[http://www.pseataskforce.org/uploads/tools/sixcoreprinciplesrelatingtosea\\_iasc\\_english.doc](http://www.pseataskforce.org/uploads/tools/sixcoreprinciplesrelatingtosea_iasc_english.doc).

Toleo hili la lugha rahisi inayosomeka imetayarishwa kwa ushirikiano kati ya jopo la IASC linaloshughulikia masuala ya Uwajibikaji kwa Watu Walioathirika na Kinga dhidi ya Unyanyasaji na Dhulma za Ngono pamoja na Watafsiri Bila Mipaka.